Powered By: www.manyamfranchise.com

SHULE YA UPILI YA WASICHANA YA GATITU

MTIHANI WA MWISHO WA MWAKA

KIDATO CHA PILI/2014

JINA.....DARASA.....NAMBARI.....

1.UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Miviga ni sherehe maalumu za kitamaduni ambazo hutendeka katika vipindi maalumu vya mwaka. Miviga hujumuisha sherehe za kuzaliwa, kuwapa watoto majina, sherehe za tohara, sherehe za ndoa na zile za maziko. Jinsi ya kusherehekea miviga hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Hata hivyo, kunayo matendo yanayoambatana na miviga ambayo hushabihiana mno miongoni mwa jamii nyingi za kiafrika.

Katika makala haya, yameonyesha matendo yenye mishabaha katika miviga ya maziko miongoni mwa jamii nyingi za kiafrika. Lengo kuu si kudhihirisha jinsi baadhi ya matendo hayo yalivyopitwa na wakati au mgongano wayo na 'ustaarabu' ama imani za kidini za kisasa, la hasha! Badala yake, yataonyesha jinsi kila tendo katika sherehe hizo ilivyochangia katika kudumisha utambulisho wa jamii husika na kuwa mfano wa saruji iliyowaunganisha wanajamii na kuendelea kuwapa matumaini. Baadhi ya mambo yatakayoshughulikiwa ni pamoja na: itikadi zilizoambatana na sherehe na maziko, mahali maalumu palipotengwa kuwazikia wafu, heshima tofauti walizopewa wafu miongoni mwa mambo mengine.

Takribani shughuli zote zilizoyazunguka maisha ya jamii za kiafrika zilikurubiana na imani fulani . Waafrika walikuwa na imani zao ambazo zilielekezwa kwa Mungu, miungu , mizimu au vitu fulani ambavyo viliaminiwa kuwa na nguvu fulani zilizodhibiti na kuyaelekeza maisha. Ithibati ya kuwepo kwa imani hizo ni kuwepo kwa maabadi maalum ambapo Waafrika walifanyia sherehe zao za ibada. Sherehe za maziko pia ziliongozwa na itikadi hizo.

Katika jamii nyingi za magharibi ya Kenya, ilikuwa lazima kwa makiwa kunyolewa nywele kipindi kifupi baada ya kumzika 'marehemu'. Sababu kuu iliyotolewa kuhusiana na hili ni kuonyesha kuanza upya kwa maisha ya marehemu 'kwingineko'. Pindi tu wafiwa walipoanza kuota nywele, ilikuwa ishara kuwa maisha ya mwendazake yameanza upya katika ulimwengu mpya. Jambo hili liliendelea kuwapa imani wanajamii juu ya 'nguvu zilizozidi nguvu' ambazo ziliushinda uwezo wao hususan zile za kifo.

Itikadi nyingine kuhusu sherehe za maziko inayofanana miongoni mwa jamii nyingi za kiafrika ni ile ya kutomzika mfu na madini yoyote; hasa vitu vilivyotengenezwa kwa vyuma au vito. Sababu mbalimbali hutolewa kuhusiana na jambo hili. Baadhi ya jamii huamini kwamba madini hayo yangekuwa kuzuizi kwa marehemu katika safari yake kuelekea katika 'ulimwengu mpya wa wafu.'

Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

Maswali

(a) Yape kichwa mwafaka makala haya. (alama 2)

.....

(b) Taja mifano matatu ya miviga (alama 3)

.....

.....

.....

(c) Taja sifa tatu za sherehe za miviga. (alama 3)

.....

.....

.....

(d) Eleza dhima tatu za kila tendo katika miviga. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

(e) Ni wapi kunathibitika kuwepo kwa imani za jamii? (alama 2)

.....

.....

.....

(f) Eleza matendo mawili yanayoonyesha kuanza upya kwa maisha ya mfu. (alama 2)

Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

.....

.....

.....

.....

(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye makala (alama 4)

(i) Ustaarabu .....

(ii) Itikadi.....

(ii) Makiwa .....

(iii) Hususan .....

2) MATUMIZI YA LUGHA

a) Sahihisha (al. 2)

Meno zake zitang'olewa kesho.

.....

b) Kitambaza hutamkiwa wapi? (al. 1)

.....

c) Weka majina yafuatayo katika ngeli zake. (al. 2)

(i) mauti.....

(ii) utukutu.....

d) Anza na shambani (al. 2)

Mzee analima shambani.

.....

e) Tambulisha matumizi ya **"po"** katika sentensi ifuatayo. (al. 2)

Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

Niliposhuka nilimwona alipokuwa.

.....

.....

f) Ainisha aina za maneno katika sentensi hii. (al. 3)

Vitatu vilipeperushwa mbali na upepo mkali.

.....

.....

.....

g) Kanusha. (al. 2)

Ukipita mtihani utakuwa shujaa mapema.

.....

h) Ainisha mofimu. (al. 3)

Zilizochomeka.

.....

.....

.....

i)Andika sentensi hii upya kwa kutumia "o " rejeshi tamati. (al. 2)

Magari ambayo huendeshwa kasi ndiyo ambayo husababisha ajali.

.....

j) Geuza katika ukubwa wingi. (al. 2)

Mtu huyo alibomoa nyumba kubwa.

.....

k) Unda nomino mbili kutokana na kitenzi **Sali.** (al. 2)

Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

.....

l)Tambua aina za vitenzi katika sentensi zifuatazo. (al. 3)

(i) Mjomba alikuwa uwanjani.

.....

(ii) Mjukuu wake ataweza kulima.

.....

m) Andika katika msemo wa taarifa. (al. 3)

"Huku ndiko mtapata maziwa yenu," mwenye duka akasema.

.....

.....

.....

.....

n) Tunga mfano mmoja wa sentensi ambatano. (al. 2)

.....

.....

o) Bainisha aina za vielezi katika sentensi ifuatayo. (al 4)

Ni nadra sana yeye kukosekana nyumbani usiku.

.....

.....

.....

p)Tunga sentensi kudhihirisha tofauti ya maneno haya. (al. 2)

(i) fuja

.....

Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

(ii) vuja

.....

q)Fafanua sifa zozote tatu za mazungumzo ya simu. (al. 3)

.....

.....

.....

3) **FASIHI SIMULIZI**

a) Taja vitanzu vyovyote vinne vya maigizo (al. 4)

.....

.....

b) Tumia miigo ya sauti ifaayo. (al. 2)

(i) Ule mti ulipopigwa na tufani ulikatika.....

(ii) Alilliangusha gunia mchangani .....

c)Eleza sifa mbili za methali (al. 2)

.....

.....

d) kamilisha methali hizi (al. 2)

(i) Kupanda mchongoma.....

(ii) Uzuri wa mkakasi.....

Powered By: www.manyamfranchise.com